



**NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL (NEMC)  
BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

**TAARIFA KWA UMMA  
MKUTANO WA WADAU KUHUSU USIMAMIZI NA UDHIBITI WA  
TAKA HATARISHI**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linawatangazia wadau wote wanaofanya biashara ya Taka hatarishi (zenye madhara)-*hazardous waste*, kuwa, utakuwapo mkutano wa wadau siku ya Jumapili Tarehe 14/ 04/2019 kuzungumzia na kujadili suala la usimamizi na udhibiti wa taka hizi hatarishi kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja.

Mkutano huu utafanyika katika ukumbi wa LAPF (*Millennium Tower*) Makumbusho, Jijini Dar es Salaam kuanzia saa 4.00 kamili asubuhi, wadau wote ikiwa ni pamoja na wakusanyaji, wanunuaji, wauzaji, wanaoingiza nchini ama kusafirishaji nje ya nchi, warejereshaji na wateketezaji taka hizo, mnaalikwa na mnaombwa kuhudhuria mkutano huu muhimu. Mamlaka mbalimbali za serikali zinazoshughulika na suala hili la Taka hatarishi pia zimealikwa. Mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. January Makamba (Mb)

Taka hatarishi (zenye madhara)-*hazardous waste* ni pamoja na vyuma chakavu, taka za kieletroniki, dutu hatarishi, mafuta machafu, taka za hospitali, Betri na Tairi zilizotumika na aina ya taka zote zinazotoka migodini. Taka hizi hatarishi zinaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira. Ili kuzuia na kudhibiti athari mbaya zitokanazo na taka zenye madhara, mfumo mahsusi unaofanya kazi kwa ufanisi wa kudhibiti taka hizi unapaswa ufuatwe kama ulivyobainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Sumu) za Mwaka 2009.

Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 na Kanuni zake. Aidha, usimamizi na udhibiti wa taka zenye madhara umebainishwa kwenye Vifungu vya 133 -139 vya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Pia Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Sumu) za Mwaka 2009 zimetoea miongozo ya kudhibiti taka sumu hapa nchini pamoja na mambo mengine yahasuyo uhifadhi wa mazingira.

Katika mkutano huo, mada inayohusu utaratibu wa kisheria kuhusu usimamizi wa taka hatarishi na changamoto zake itawasilishwa na wadau watapata fursa ya kuchangia maoni juu ya masuala ya ukusanyaji, usafirishaji, urejereshaji na uteketezaji wa taka hatarishi ili kufikia uelewa wa pamoja juu ya suala hili.

***Taarifa hii imetolewa na:***

***Mkurugenzi Mkuu ,  
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)***

***Na kusambazwa na:***

***Kitengo cha Habari, Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma,  
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),  
Plot No. 28, 29 & 30-35 Regent Street, P.O. Box 63154, Dar es Salaam.  
Simu: +255 22 2774889, Direct line: +255 22 2774852 Mobile: 0713 608930/ 0692108566  
Fax: +255 22 2774901, Email: dg@nemc.or.tz***